

# MUHTASARI WA MATOKEO MUHIMU YA UTAFITI WA MNYORORO WA THAMANI YA MKAA MKOANI TANGA, 2024



## 1. Utangulizi

Shirika la TFCG ([www.tfcg.org](http://www.tfcg.org)) kwa kushirikiana na MJUMITA, chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya, wanatekeleza Mradi wa IFBEST katika vijiji 13 vya Wilaya za Kilindi, Handeni, Mkinga, na Pangani. Utafiti huu wa Mei–Juni 2024 ulilenga kutathimini gharama, bei, na changamoto za biashara ya mkaa katika masoko ya Zanzibar, Dar es Salaam, na Arusha.

## 2. Matokeo Muhimu.

### 2.1 Muundo wa Gharama na Mapato

Gharama za kudumu zinahusisha ada za leseni na vibali kwa halmashauri (TZS 270,000–300,000 kwa mwaka). Gharama zinazobadilika ni pamoja na ununuzi wa mkaa (TZS 8,000–17,500 kwa gunia), usafirishaji (TZS 13,000 kwa gunia), na mrabaha (TZS 12,500–25,000 kwa gunia).

## 2.2 Soko la Zanzibar

Wafanyabiashara wa Zanzibar wanapata faida ndogo (TZS 304 kwa gunia) kutohata na gharama kubwa za usafirishaji na ada. Wengi wao hukwepa malipo ya ada na ushuru, hali inayodhoofisha uendelevu wa biashara.

## 2.3 Masoko ya Dar es Salaam na Arusha

Masoko haya yanaonyesha faida ya 14% kwa Dar es Salaam na 12% kwa Arusha. Magunia makubwa ya mkaa yanapendelewa zaidi na biashara inakua kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

## 2.4 Wilaya ya Kilindi

Biashara ya mkaa Kilindi haiko rasmi, wafanyabiashara wengi hawajasajiliwa. Vijiji kama Mswaki, Mapanga, na Mmbogo havina wafanyabiashara waliosajiliwa, lakini mkaa huzalishwa na kuuzwa kuititia njia zisizo rasmi.

## 3. Hitimisho na Mapendekezo

Utafiti huu umebaini changamoto za kimfumo katika mchakato wa mpito kuelekea uzalishaji endelevu wa mkaa. Bei ya chini ya mkaa, ukwepaji wa ada na ushuru, na faida ndogo vinahatarisha uendelevu wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM), hasa katika biashara ya Zanzibar. Ingawa masoko ya Dar es Salaam na Arusha yanaonekana kuwa na matumaini Zaidi.

### 3.1 Ili kuboresha uendelevu, hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa:

- Kukabiliana na ukwepaji wa ada na ushuru katika minyororo ya thamani ya mkaa nje ya mfumo wa CBFM.
- Kuwezesha jamii kuwa na uhuru wa kuweka bei ya ushuru wa mkaa kwa kurekebisha Tangazo la Serikali No. 417 (2019) na 59 (2022).
- Kuongeza mchango wa biashara za misitu katika uchumi wa taifa kwa kupanua biashara endelevu za misitu katika Hifadhi za Misitu za Ardhi ya Vijiji na kuanzisha Misitu ya vijiji zaidi.
- Kuhakikisha mkaa wote unavunwa kwa njia endelevu.



Funded by the  
European Union

